ISSN 0856–034X

Supplement No. 23 *22nd July, 2011*

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 29 Vol. 92 dated 22nd July, 2011

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 194 la tarehe 22/7/2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA STENDI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA MAGU ZA MWAKA, 2011

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Wilaya ya Magu, 2011 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"Afisa Mdhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Magu;

"Mabasi" maana yake ni magari yote yanayosafirisha abiria ila hayahusishi taksi;

"Mabasi makubwa" ni mabasi yanayobeba abiria 25 na kuendelea;

"Mabasi madogo" ni mabasi yenye uwezo wa kubeba abiria chini ya 25;

"Mmiliki" maana yake ni mtu mwenye gari, dereva, kondakta au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na mwenye gari kuwa na mamlaka ya kumiliki wakati anapita stendi;

"Stendi" maana yake ni kituo cha stendi kuu ya mabasi ya Magu;

"Wakala" maana yake ni Chama cha Ushirika, Kampuni, Afisa wa Halmashauri au mtu binafsi atakayeteuliwa kwa maandishi na Halmashauri kukusanya mapato ya Halmashauri;

Stendi

4.–(1) Halmashauri inaanzisha stendi maalum kwa ajili ya magari ya abiria, ambayo itatumika na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni wajibu wa wamiliki wa mabasi yote yatokayo na kuelekea Mwanza Mjini au Kwimba, Lamadi, Bunda, Musoma, Sirari, Tarime na Nchi jirani ya Kenya pamoja na maeneo mengine ambayo hayakutajwa na Sheria Ndogo hizi kuhakikisha kwamba magari yao yanaingia stendi kuu ya mabasi ya Magu mjini.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kupakia na kushusha abiria katika eneo ambalo siyo stendi;

(b) kupiga debe katika eneo la stendi.

Ushuru

5.–(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa gari la abiria anayekusudia kupakia au kushusha abiria katika eneo la stendi kulipa ushuru kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru huo utalipwa gari linapotoka stendi kuendelea na safari zake.

Uvaaji wa sare

6. Itakuwa ni wajibu wa Mawakala wote wa Mabasi wanaojihusisha na uuzaji wa tiketi sehemu ya stendi kuvaa sare na vitambulisho vitakavyowatambulisha kuwa wao ni mawakala.

Uwezo wa kukamata

7.–(1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kukamata na kuzuia gari lolote ambalo halijalipiwa ushuru.

(2) Gari lolote lililokamatwa au kuzuiliwa litahesabiwa kama lililotelekezwa, na Halmashauri itatoza shilingi elfu hamsini kwa kila siku ikiwa ni gharama ya kutunza gari hilo mpaka hapo mmiliki wake atakapolipa ushuru anaodaiwa pamoja na gharama za kutunza gari hilo

8. Itakuwa ni marufuku kwa gari lolote kushusha abiria na mizigo nje ya eneo la stendi.

Wajibu wa wakala

9. Wakala aliyeteuliwa kukusanya ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kutoza ushuru kwa viwango vilivyoainishwa;

(b) kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusiana na magari yaliyokiuka taratibu zilizowekwa na Sheria Ndogo hizi.

Makosa

10. Mtu yeyote ikiwa ni Dereva, kondakta au mmiliki:-

(a) atakayekataa kuingiza gari lake ndani ya stendi au;

(b) atakayesimama kupakia au kushusha abiria nje ya stendi au;

(c) atakayekataa au kukwepa kulipa ushuru wa stendi.;

Atakuwa ametenda kosa.

Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

JEDWALI

Aina ya Gari	*Kiasi cha Ushuru*
(a) Mabasi Makubwa	1500/=
(b) Mabasi Madogo	1000/=
(c) Taxi	500/=

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio liliilopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu uliofanyika tarehe 28 mwezi 05 mwaka 2010 mbele ya:–

CORNEL E. N
Mkurugenzi M
Halmashauri ya Wilaya

L.S.

DESTERY B.
Mwenyekiti wa Haln
Halmashauri ya Wilaya

NAKUBALI

Dodoma, 26 Mei 2011

MHE. MIZENGO P. PINI
Waziri

TANGAZO LA SERIKALI NA. 195 la tarehe 22/7/2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA W
MAGU ZA MWAKA, 2011

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndo za (wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Magu za mwaka zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Seri

Eneo la matumizi
Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halm ya Wilaya ya Magu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vingi "Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halm aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.;

"Mazao" ni mazao ya kilimo yanayozalishwa katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika lolote linalonunua mazao ndani ya Halmashauri;

"Ushuru" maana yake ni fedha itakayolipwa na mnunuzi kama ushuru wa mazao;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kampuni au Taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya Ushuru kwa niaba yake.

Ushuru wa mazao

4.–(1) Halmashauri inaanzisha ushuru wa mazao utakaotozwa kwa mazao yatakayozalishwa katika eneo la Halmashauri.

(2) Ushuru huo utalipwa na mnunuzi kwa masharti yaliyoainishwa na Sheria Ndogo hizi.

(3) Baada ya kulipa ushuru mnunuzi atawajibika kudai risiti yenye muhuri na Nembo ya Halmashauri na atawajibika kuionyesha kwa Afisa Muidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(4) Ushuru wa Mazao utakaotozwa ni asilimia tatu (3%) ya bei ya mauzo ya soko.

Uteuzi wa wakala

5.–(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, Kampuni au Taasisi kuwa wakala wa kukusanya Ushuru kwa masharti yaliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni wajibu wa kila mnunuzi au wakala wake kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu mazao aliyonunua.

(3) Kila Meneja, Mkurugenzi au mtu yeyote mwenye dhamana ya usimamizi wa kiwanda, shirika, chama cha ushirika anaweza kutangazwa kuwa wakala chini ya Sheria Ndogo hizi.

Usimamizi wa masoko

6.–(1) Masoko yote ndani ya eneo la Halmashauri yatakuwa chini ya Afisa soko ambaye atasimamia uendeshaji wa masoko hayo.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi, muuzaji au mtu ye kumzuia Afisa soko au Afisa Muidhiniwa kusimamia utekeleza Sheria Ndogo hizi.

Uanzishaji wa masoko vijijini

7.–(1) Kila Kijiji ndani ya Halmashauri kitatenga eneo maa ajili ya kuuzia mazao ambapo kila muuzaji atauzia mazao yak eneo hilo.

(2) Wanunuzi wote wa mazao watanunua mazao hayo kat lilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa mazao na si vinginevyo.

Muda wa kusafirisha mazao

8. Ni marufuku kwa mnunuzi yeyote kusafirisha mazao b saa 12:00 Jioni na kabla ya saa 1:00 asubuhi.

Makosa

9.–(1) Itakuwa ni kosa kwa mnunuzi yeyote

(a) kusafirisha mazao baada ya saa 12:00 jioni na k Saa 1:00 asubuhi;

(b) kusafirisha mazao aliyonunua kabla ya kulipa Ush

(c) kukataa au kukwepa kulipa ushuru;

(d) kukataa kuonyesha risiti aliyolipia ushuru kw Muidhiniwa;

(e) kumpa mtu, kampuni au wakala mwingine kibali c

(2) Itakuwa ni makosa kwa muuzaji yeyote:

(a) kuuza mazao katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(b) kufanya jambo lolote litakalosababisha kukwepa ushuru;

(3) Itakuwa ni kosa kwa wakala yeyote:-

(a) kuchelewa kuwasilisha Ushuru kwa Halmashauri;

(b) kutoa taarifa za uongo kuhusu idadi ya w wa ushuru;

(c) kuwasilisha kwa Halmashauri kiwango kidogo ch kinyume na makubaliano; na

(d) kumshawishi mtu yeyote, kundi la watu au taasisi w ushuru.

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi a ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyozidi shilin hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adha mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo

JEDWALI

Na	*Aina ya Mazao*	*Kiasi cha Ushuru*
1.	Mahindi	3%ya bei ya mauzo ya soko
2.	Maharage	3% ya bei ya mauzo ya soko
3.	Ulezi	3% ya bei ya mauzo ya soko
4.	Uwele	3% ya bei ya mauzo ya soko
5.	Dengu /choroko	3% ya bei ya mauzo ya soko
6.	Mihogo/Udaga	3% ya bei ya mauzo ya soko
7.	Mchele	3% ya bei ya mauzo ya soko

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu uliofanyika tarehe 28 mwezi 05 mwaka 2010 mbele ya:–

L.S.

CORNEL E. NGUDU-NGI.
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Magu

DESTERY B. KISWAGA,
Mwenyekiti wa Halmashauri
Halmashauri ya Wilaya ya Magu

NAKUBALI

Dodoma,
26 Mei, 2010

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB.),
Waziri Mkuu

TANGAZO LA SERIKALI NA. 196 la tarehe 22/7/2011

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu vya 7 (1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU) ZA MWAKA 2011

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kwa jina la Sheria Ndogo za (A Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Magu 2011 na zitaanza kut mara baada ya kutangazwa kwenye *Gazeti* la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmasha Wilaya ya Magu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakapoelezwa vingine -"Afisa muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusi utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Magu;

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo ya fedha yanayotoz Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya huduma mbal zitolewazo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Ha' ashi Wilaya ya Magu pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kute majukumu ya Mkurugenzi;

"Mkusanya ushuru" maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteul Halmashauri kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria ndogo l

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa S 290.

Ushuru wa mazao

4.–(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya hu mbalimbali, vibali na leseni zitolewazo kama ilivyoainishwa k sehemu (i) – (viii) ya Jedwali B la SheriaNdogo hizi.

(2) Ada na ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utatakiwa kulipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Baada ya malipo kufanyika Halmashauri itatoa stakabadhi yenye muhuri na nembo ya Halmashauri sawa na ushuru uliolipwa.

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada na ushuru kuhakikisha analipa ada au ushuru kama ilivyoelekezwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi. Wajibu wa kulipa ushuru

6.–(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mbao za matangazo kwa viwango vilivyotajwa katika Jedwali A la Sheria Ndogo hizi. Ushuru wa mbao za matangazo

(2) Matangazo yanayotolewa kwa mujibu wa masharti yaliyomo kwenye sheria za makampuni hayatatozwa ushuru uliowekwa na Sheria Ndogo hizi.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka mbao za matangazo katika sehemu yoyote ndani ya eneo la Halmashauri bila kulipa ada au ushuru.

(4) Halmashauri itatoa kibali cha kuweka mbao za matangazo baada ya kupokea maombi kutoka kwa mtu binafsi, taasisi na kampuni na uthibitisho wa malipo ya ada au ushuru kufanyika.

7–(1) kila mnyama aliyechinjwa kwenye machinjio ndani ya eneo la Halmashauri atalipiwa ushuru wa ukaguzi wa nyama na ushuru wa machinjio kwa viwango kama ilivyoainishwa kwenye jedwali B la Sheria Ndogo hizi. Ushuru wa machinjio, ngozi na ukaguzi wa nyama

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutoza ushuru wa ukaguzi wa nyama kwa wanyama wachinjwao vijijini.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi wa ngozi ndani ya eneo la Halmashauri kulipia ushuru wa ngozi kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Kodi ya pango mali za Halmashauri

8.–(1) Kila mpangaji kwenye nyumba au kibanda kinachom: Halmashauri atatakiwa kulipa kodi ya pango la nyumba au kiba kwa viwango vilivyoonyeshwa kwenye sehemu (iii) ya jedwali B Ndogo hizi.

(2) Wapangaji wa nyumba za Halmashauri isipokuwa kwa w wa Halmashauri watatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri kuingia kwenye nyumba hizo.

(3) Halmashauri itaweka utaratibu wa upangaji wa vibanda sc sehemu nyingine yoyote iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa vibanc kwa kusaini mkataba.

Uteuzi wa wakala

9.–(1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kaa au k kuwa wakala wa kukusanya ada na ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa wakala

(2) Wakala atakayeteuliwa atawajibika:-

(a) kutoa taarifa ya maandishi juu ya orodha ya wanaotakiwa kulipa ada au ushuru ndani ya eneo au s ya eneo ambapo ameteuliwa kukusanya ushuru;

(b) kukusanya na kupokea ada na ushuru kutoka kwa ki anayedaiwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hi

(c) kuwasilisha pesa zote alizokusanya kwa Halmashau mujibu wa Mkataba;

(d) kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa ya jina la mtu y atakayeshindwa kulipa kiasi cha ada au us anachodaiwa.

Makosa kwa wakala

(3) Wakala yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

(a) atashindwa kuwasilisha kwa Halmashauri kiasi choc cha ada au ushuru alichokusanya; au

(b) kwa kufahamu atamtoza mtu yeyote kiasi cha ad ushuru zaidi ya kile kilichoainishwa chini ya Sheria Nd hizi.

Makosa na adhabu

10.–(1) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo l atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikan hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atatumi

kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa chini ya kifungu cha (1) mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi elfu hamsini baada ya mtu huyo kukiri kosa kwa maandishi kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika jedwali C la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI A

USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO YA BIASHARA

1. Matangazo ya (promotion).....	Sh. 50,000/=kwa siku
2. Matangazo ya biashara yasiyowaka (10.000cm²)..	Sh. 50,000/= kwa miezi sita
3. Matangazo ya biashara kwa kila mita za miraba.....	Sh. 10,000/= kwa miezi sita
4. Matangazo ya biashara (pande mbili kwa kila mita za mraba (m²).....	Sh. 20,000/= kwa miezi sita
5. Matangazo ya kutumia vitambaa (cloth banners) upande mmoja.....	Sh. 10,000/= kwa miezi sita
6. Matangazo ya kutumia vitambaa (cloth banners) pande mbili.....	Sh. 20.000/= kwa mwezi

---

JEDWALI B

Sehemu (i)

Ushuru wa mifugo Mnadani

1. Ng'ombe.....	Sh. 2,000/= kwa kila ng'ombe
2 Kondoo.....	Sh. 1,000/= kwa kila kondoo
3. Mbuzi	Sh. 1,000/= kwa kila mbuzi
4. Nguruwe.....	Sh. 1,000/= kwa kila nguruwe

Sehemu (ii)

Ada ya kukodi Lori, Greda na Roller

1. Ada kwa kutumia Lori la Halmashauri	Sh. 80,000/= kwa siku
2. Ada ya kutumia Roller ya Halmashauri.....	Sh. 150,000/= kwa siku
3. Ada ya kukodisha Greda.....	Sh. 500,000/= kwa siku

Schemu ya (iii)

Ada ya kutumia mali za Halmashauri

1. Nyumba za Halmashauri zenye vyumba vitatu zilizopo mtaa wa NHC..... Sh. 25,000/= kv
2. Nyumba aina nyinginezo za vijijini..... Sh. 5,000/=
3. Nyumba za Halmashauri zenye vyumba viwili zilizopo mtaa wa NHC..... Sh. 15,000/= kv
4. Nyumba za Halmashauri zenye vyumba vitatu zilizopo vijijini ..... Sh. 15,000/= kv
5. Nyumba za Halmashauri zenye vyumba viwili zilizopo vijijini..... Sh. 10,000/= kv
6. Ada ya vibanda vya biashara kuzunguka stendi kuu ya mabasi..... Sh. 20,000/= kv
7. Ada ya vibanda vya biashara kuzunguka soko kuu la Magu mjini..... Sh. 15 /= kv

Sehemu (iv)

Ada ya minada ya magulio

8. Ada ya mfanyabiashara yoyote ile kwa kuuza bidhaa yoyote ile itakayouzwa mnadani kwenye eneo la minada au magulio.....Sh. 1,500/= kv

Sehemu ya (v)

Wafanyabiashara katika soko kuu

9. Wauza mboga..... Sh. 200 kwa siku
10. Wauza bidhaa mchanganyiko ..... Sh. 300 kwa siku
11. Ada ya kutumia vyoo vya umma..... Sh. 200 kwa haja kubwa au
12. Masoko mengineyo..... Sh. 200 kwa siku

Sehemu (vi)

Ada ya wafanyabiashara wa mitumba

13. Wafanyabiashara wote wa mitumba nje ya maeneo ya magulio .....Shs.. kwa

Sehemu (vii)

Ada kwa biashara nyinginezo

14. Fundi viatu/mpira/viatu rangi..... Sh. 3,000/= kwa mwaka
15. Fundi cherehani..... Sh. 3,000/= kwa mwaka
16. Fundi baiskeli..... Sh. 2,000/= kwa mwaka
17. Dobi..... Sh. 2,000/= kwa mwaka

18. Fundi radio.....Sh. 12,000/= kwa mwaka
19. Fundi saa.....Sh. 2,000/= kwa mwaka
20. Kinyozi.....Sh. 12,000/= kwa mwaka
21. Mikokoteni .....Sh. 2,000/= kwa mwaka
22. Migahawa ya vyakula.....Sh. 10,000/= kwa mwaka
23. Saluni za wanawake.....Sh. 12,000/= kwa mwaka

Sehemu (viii)

Ushuru wa Samaki .....Asilimia 4 ya bei kwa kilo

JEDWALI C

HATI YA KUKIRI MAKOSA
(CHINI YA KIFUNGU CHA 13)

Mimi .....nakiri mbele ya .....Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Magu kwamba mnamo tarehe .....ya mwezi .....mwaka.....nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha .....cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Magu za mwaka 2010 nipo tayari kulipa kiasi cha ada/ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu kilichotajwa hapo juu.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe.....

Sahihi.....

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu uliofanyika tarehe 28 mwezi 05 mwaka 2010 mbele ya:–

CORNEL E. NGUDU-NGI,
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Magu

L.S.

DESTERY B. KISWAGA,
Mwenyekiti wa Halmashauri
Halmashauri ya Wilaya ya Magu

NAKUBALI

MHE. MIZENGO P. PINDA (MB.),
Waziri Mkuu

Dodoma,
26 Mei, 2010

TANGAZO LA SERIKALI NA. 197 la tarehe 22/7/2011

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA (MAM ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARAZA) ZA HALMASHAURI YA YA MAGU) ZA MWAKA 2011

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (wa Baraza) za Halmashauri ya Wilaya ya Magu za mwaka zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Seri

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lilipo chini ya r ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vingine

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halm aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hi

"Baraza" maana yake ni eneo lilipo mbele ya jengo na ni pa...oja lilipo kati ya ukuta wa jengo na barabara;

"bidhaa za biashara" maana yake ni bidhaa au mali zilizotolewa ku nje kwa nia ya kuuzwa au kubadilishwa;

"Halmashauri: ina maana ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu;

"Mkurugenzi" ina maana yake Mkurugenzi Mtendaji wa Halm ya Wilaya ya Magu pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kut majukumu ya Mkurugenzi.

Tangazo la Serikali Na. 197 (linaendelea)

(d) atashindwa au atakataa kuweka au kuwasha baraza la jengo lake.

7. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sh hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atat isiyopungua shilingi elfu thelathini na isiyozidi shilingi elfu kutumikia kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili k yaani faini na kifungo.

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu umebandik Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye m Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu t tarehe 28 mwezi 05 mwaka 2010 mbele ya:-

CORNEL E. M
Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya

L.S.

DESTERY B.
Mwenyekiti wa Ha
Halmashauri ya Wilaya

NAKUBALI

MHE. MIZENGO P. PIN
Waz

Dodoma,
26 Mei, 2010

TANGAZO LA SERIKALI NA. 198 la tarehe 22/7/2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA. 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 1(

SHERIA NDOGO ZA (UANDIKISHWAJI WA TEKSI) (MAREKEBISHO
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI ZA MWAKA, 2011

1. Sheria Ndogo hizi ztaitwa Sheria Ndogo za (Uandikish Teksi) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Hai za mwa